TANGAZO LA SERIKALI NA. 560 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MIALO NA USHURU WA SAMAKI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA ZA MWAKA, 2024.

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Mialo na Ushuru wa Samaki ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga za mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Kamati" maana yake ni kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi iliyoteuliwa kusimamia shughuli za uvuvi endelevu katika kambi chini ya Sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake;

"kambi" maana yake ni eneo linalotambulika na Halmashauri kwa shughuli za uvuvi;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi;

"mwalo" ni kambi inayotambulika na iliyoruhusiwa kuendesha shughuli za uvuvi ndani ya Wilaya ya

Igunga;

"wakala" maana yake ni mtu wa mtu, Taasisi, Kampuni au kikundi cha watu walioteuliwa na Halmashauri kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa kwenye samaki na mazao ya samaki;

"mnada" maana yake ni mahali katika mwalo palipotengwa na Halmashauri kwa kusudi la kuuzia samaki baada ya kuvuliwa;

"samaki" kwa mujibu wa kanuni hii itajumuisha dagaa; na

"zana za uvuvi" maana yake ni nyavu za kuvulia, Ndoano, Migono mitego na zana zote zinazokubalika kisheria.

Mialo ya samaki

4.-(1) Halmashauri itatambua na kusajili uongozi wa mialo yote.

(2) Mialo itatambulika kwa kanda, ambazo zitajulikana kwa majina ya vitongoji husika kama itakavyoamuliwa na kikao cha pamoja kati ya Mkurugenzi na kamati.

Usimamizi wa mialo

5.-(1) Halmashauri inaweza kusitisha shughuli za uvuvi katika Mialo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe 1 mwezi Januari hadi tarehe 31 mwezi Machi kila mwaka kwa lengo la kuchochea ongezeko la samaki.

(2) Halmashauri inaweza kukamata samaki wa mtu yeyote ambaye atakamatwa akiendesha shughuli za uvuvi ndani ya kipindi ambacho shughuli za uvuvi zitasitishwa.

(3) Endapo mmiliki au mvuvi wa samaki waliokamatwa atasindwa kutimiza masharti ya Sheria ndogo hii ndani ya siku moja kwa samaki, Halmashauri baada ya kupata amri ya Mahakama itauza samaki, na fedha zitakazopatikana zitatumika kulipia gharama zote Halmashauri ilizoingia katika ukamataji, kutunza na zoezi la mnada na ushuru utakaokuwa unadaiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(4) Halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa samaki na zana za uvuvi zilizoharibika kutokana na kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria Ndogo hii isipokuwa pale ambapo itathibitika kuwa ni uzembe wa watumishi wake.

Kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi

6.-(1) Halmashauri kwakushauriana na serikali ya Kijiji ambapo kuna mialo ya uvuvi wa samaki itaunda kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi kwaajili ya kusimamia mialo hiyo.

(2) Kamati iliyoundwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa kamati, ambaye atakuwa ni mwenyekiti wa kitongoji husika ambapo mwalo huo wa samaki unapatikana,
(b) Katibu wa kamati, ambaye atakuwa ni kiongozi wa kambi.
(c) Mtendaji wa kijiji husika, ambaye atakuwa ni mwenyekiti wa kamati hiyo,
(d) Wavuvi watatu kutoka katika uongozi wa wavuvi; na
(e) Wafanyabiashara wawili watakao pendekezwa na Mwenyekiti wa Wafanyabiashara.

(3) Mjumbe aliyehama au kuondoka katika eneo la mwalo husika kwa muda wa siku 90 na kuendelea, au aliyeondolewa na mkurugenzi ataondolewa kwenye nafasi yake na utaratibu wa kuwapata wajumbe kwa mujibu wa kanuni hii utatumika kujaza nafasi ya mjumbe huyo.

Majukumu ya kamati

7. Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuanzisha rejesta ya wavuvi, vyombo vya uvuvi na kuruhusu zana za uvuvi zinazokubalika kisheria;
(b) kushirikiana na afisa mwidhiniwa au wakala anaefanya ukaguzi wa zana za uvuvi; na
(c) kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kwa Mkurugenzi kila baada ya miezi mitatu.

Muda wa kamati

8. Wajumbe wa kamati watahudumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu kuteuliwa kwao.

(2) Wajumbe wa kamati wanaweza kuteuliwa tena kwa kadri Mkurugenzi kwa kushauriana na serikali ya Kijiji atavyoona inafaa.

(3) Mkurugenzi anaweza kwa kushauriana na serikali ya Kijiji kumwondoa katika kamati mjumbe ambaye

atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hii.

Uwasilishaji wa taarifa za mitumbwi

9. Kila mmiliki wa mtumbwi au muwakilishi wake wake atahakikisha anawasilisha taarifa za usajili wa mtumbwi wake kwa kamati ya usimamizi wa rasilimali ya uvuvi siku saba tangu alipopata usajili wa mtumbwi huo.

Ushuru wa Samaki

10.-(1) Halmashauri itakusanya ushuru wa samaki kama ulivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya kanuni hii utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza, ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(3) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(4) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, mtu kudai kuwa amelipa ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Wajibu wa kulipa Ushuru

11. Mtu yeyote anayestahili kulipa ushuru atatakiwa kulipa ushuru huo kabla ya kuondoka kwenye mwalo na kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Eneo la upimaji

12. Halmashauri itatenga eneo katika mwalo kwaajili ya upimaji wa Samaki waliovuliwa na Samaki wote watapaswa kupelekwa kwenye eneo hilo kwaajili ya upimaji.

Muda wa mnada

13. Mnada wa samaki utafunguliwa kuanzia saa moja na nusu asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

Muda wa kusafirisha Samaki

14.-(1) Muda wa kusafirisha samaki kutoka mnadani kwenye mialo iliyotengwa na Halmashauri kwa shughuli hizo ni kuanzia saa moja na nusu asubuhi na mwisho ni saa kumi na mbili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) samaki wanaweza kusafirishwa nje ya muda uliotajwa kwa

kibali maalum cha Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa kutoka katika eneo la mwalo husika.

Uteuzi wa Wakala

15.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na
(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa

16.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ushuru au atamsaidia mtu mwingine asilipe ushuru;
(b) atafanya hesabu za uongo kwa kupunguza ushuru isivyo halali;
(c) atatoa taarifa za uongo kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri wajibu wake au wa mtu mwingine kulipa ushuru;
(d) ataandaa na kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa hesabu au kumbukumbu za uongo ambazo zinaweza kuathiri ukokotoaji wa ushuru;
(e) atamzuia au kujaribu kumzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake;
(f) ataharibu kwa makusudi au kwa uzembe taarifa au mfumo wa taarifa za hesabu;
(g) ataharibu kwa makusudi au kwa uzembe vitendea kazi vya kukusanyia ushuru;
(h) atauuza au kununua samaki nje ya mnada uliotengwa kwa ajili ya mauzo ya samaki;
(i) atauza au kununua samaki zaidi ya muda uliopangwa;
(j) atakutwa nje ya mwalo akisafirisha samaki bila

kulipia ushuru; au

(k) atatenda jambo lolote kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii.

Adhabu

17. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya Kifungu chochote katika Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki mbili na kisichozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

18. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(1))*

USHURU WA SAMAKI

| Namba | Aina ya Samaki | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) kwa Kilo |
|---|---|---|
| 1. | Perege | 150/= |
| 2. | Kambare | 150/= |
| 3. | Kamongo | 150/= |
| 4. | Dagaa | 100/= |
| 5. | Samaki wengine ambao hawajatajwa | 100/= |

____________

JEDWALI LA PILI

____________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya Aya ya ……..ya Sheria Ndogo za Usimamizi wa Mialo na Ushuru wa Samaki za Halmashauri ya Wilaya ya Igunga za Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi……………………………………………………………………. badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ....................................................
MBELE YA:
Jina……................................................
Wadhifa: ..................................................
Saini: ..................................................
Tarehe: ...............................................

*Tangazo la Serikali Na. 560 (Linaendelea)*

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya wilaya ya Igunga uliofanyika tarehe 11 mwezi Agosti Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

SELWA ABDALLA HAMID
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Igunga*

LUCAS MOGA BUGOTA
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Igunga*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
13 Mei, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Tamisemi*